




**NOOR**  
International

# **Ushahidi wa Tawhidi na Haki ya Mwenyezi Mungu**

Njia ya Uislamu katika  
Kujitakasa na  
Kukabiliana  
na Changamoto



**noor.gallery**



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

● **Kwa jina la Allah Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu** ●

إِلَّا اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ لَا تَأْخُذُهُ سِنَّةٌ وَلَا نَوْمٌ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَا يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ ﴿٢٥٥﴾

[سورة البقرة: ٢٥٥]

Allah, hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Yeye tu. Yeye ndiye Mwenye uhai wa milele, Mwenye kusimamia kila kitu. Hapatwi na kusinzia wala kulala. Ni vyake yeye tu vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Ni nani awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao, wala hawajui kitu katika elimu yake isipokuwa atakacho tu. Kursi yake imezienea mbingu na ardhi wala hakumchoshi kuzihifadhi (mbingu, ardhi na vilivyomo), na Yeye ndiye aliye juu na ndiye aliye Mkuu

Qurani (2:255)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



هَيَوْمَ تَرَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ يَسْعَى نُورُهُمْ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ  
 وَبِأَيْمَانِهِمْ بِشَرِّكُمْ الْيَوْمَ جَنَّتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ  
 فِيهَا ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٢﴾ يَوْمَ يَقُولُ الْمُنْفِقُونَ وَالْمُنَافِقَاتُ  
 لِلَّذِينَ ءَامَنُوا انظُرُونَا نَقْتَبِسْ مِنْ نُورِكُمْ قِيلَ ارْجِعُوا وَرَاءَكُمْ  
 فَالْتَمِسُوا نُورًا فَضُرِبَ بَيْنَهُم بِسُورٍ لَهُ وَبَابٌ بَاطِنُهُ فِيهِ الرَّحْمَةُ  
 وَظَاهِرُهُ مِنْ قِبَلِهِ الْعَذَابُ ﴿١٣﴾

[سورة الحديد: ١٢-١٣]

Siku utakayowaona Waumini wa kiume na Waumini wa kike,  
 nuru zao zinakimbilia mbele yao na kuliani kwao;  
 (wataambiwa): Bishara njema kwenu leo! Ya pepo zipitazo  
 chini yake mito, ni wenye kukaa humo milele. Huko ndiko  
 kufuzu kukubwa Siku wanafiki wa kiume na wanafiki wa kike  
 watakapowaambia wale walioamini: Tungojeeni, tupate  
 mwangaza kutokana na nuru yenu! (Wataambiwa): Rudini  
 nyuma yenu, na mtafute huko nuru (yenu)! Kisha utawekwa  
 ukuta baina yao wenye mlango, ndani mna rahma na nje kwa  
 upande wake wa mbele mna adhabu

Qurani (57:12-13)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA - KLICKEN



﴿وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ وَنَعَلْمُ مَا تُوسْوِسُ بِهِ  
نَفْسُهُ ۗ وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ ﴿١٦﴾﴾

[ سورة ق : ١٦ ]

Na kwa yakini Tumemuumba Mtu na  
Tunajua yale inayowaza nafsi yake, na  
Sisi Tuko karibu naye kuliko mshipa  
wa shingoni mwake

Qurani (50:16)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي  
الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ  
يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٩٠﴾

[النحل: ٩٠]

Kwa hakika Allah anaamuru uadilifu, na  
ihsani, na kuwapa (sadaka) ndugu wa  
karibu na anakataza uchafu, na uovu, na  
uasi. Anawanasihini ili mpate kukumbuka

Qurani (16: 90)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا  
وَإِذَا حَكَمْتُمْ بَيْنَ النَّاسِ أَنْ تَحْكُمُوا بِالْعَدْلِ إِنَّ اللَّهَ  
نِعِمَّا يَعِظُكُمْ بِهِ إِنَّ اللَّهَ كَانَ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٥٨﴾

[النساء: ٥٨]

Hakika, Allah anakuamrisheni kurudisha  
amana kwa wenyewe, na mnapo hukumu  
baina ya watu mhukumu kwa uadilifu.  
Hakika, mazuri mno anayokuwaidhini  
Allah ni hayo. Hakika Allah ndiye Mwenye  
kusikia, Mwenye kuona

Qurani (3: 58)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA





NOOR  
International

هَيَّا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ  
وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَا نُ قَوْمٍ عَلَىٰ أَلَّا تَعْدِلُوا اعْدِلُوا هُوَ أَقْرَبُ  
لِلتَّقْوَىٰ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٨﴾

[سورة المائدة: ٨]

Enyi miloamini, kuweni wasimamizi (wa haki) kwa ajili ya Allah, mtoao ushahidi kwa uadilifu.

Na kuwachukia (watu) kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu (kwa watu wote). Hilo ndilo lililo karibu zaidi (kufikisha) kwenye uchamungu. Na mcheni Allah. Hakika, Allah anayajua mnayoyatenda

Qurani (5:8)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



هَقُلْ يَتَوَفَّنَا مَلَكُ الْمَوْتِ الَّذِي وُكِّلَ  
بِكُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴿١١﴾

[السجدة: ١١]

**Sema: Atakufisheni Malaika wa mauti  
aliye wakilishwa juu yenu; kisha  
mtarejeshwa kwa Mola wenu Mlezi**

Qurani (32: 11)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



هَلْ قَدْ أَفْلَحَ مَنْ زَكَّاهَا ﴿٩﴾ وَقَدْ  
خَابَ مَنْ دَسَّاهَا ﴿١٠﴾

[الشمس: ٩-١٠]

Hakika amefanikiwa aliye itakasa,  
Na hakika amepata hasara aliye  
iviza (ichafua)

Qurani (91: 9-10)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا  
وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾

[الإنسان: ٣]

Hakika, sisi tumemuongoza (tumempa  
mwongozo unaofikishwa na Mitume);  
ama awe mwenye kushukuru au mwenye  
kukufuru

Qurani (76:3)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



وَأَقِيمُوا الْوَزْنَ بِالْقِسْطِ وَلَا  
تُخْسِرُوا الْمِيزَانَ ﴿٩﴾

[الرحمن: ٩]

Na simamisheni mzani kwa  
uadilifu na msipunguze mizani

Qurani (55:9)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ وَإِن تَكُ حَسَنَةً يُضْعِفْهَا وَيُؤْتِ مِنْ لَدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾

[النساء: ٤٠]

Hakika, Allah Hadhulumu uzito wa punje. Na kama (uzito huo wa punje) ni jambo zuri analizidisha na anatoa ujira mkubwa kabisa kutoka kwake

Qurani (4:40)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA

